# Cha.ki.ta

**CHAMA CHA KISWAHILI CHA TAIFA-KENYA**

**KATIBA YA CHAMA CHA KISWAHILI CHA TAIFA-KENYA**

# Cha.ki.ta

**CHAMA CHA KISWAHILI CHA TAIFA-KENYA**

**KATIBA YA CHAMA CHA KISWAHILI CHA TAIFA-KENYA**

## KIFUNGU CHA I

**JINA**

Jina la chama ni CHAMA CHA KISWAHILI CHA TAIFA-KENYA, kitakachorejelewa katika hii katiba kama **CIIAKITA.**

CHAKITA ni chama ambacho hakijihusishi na maswala ya kisiasa wala shughuli za kujipatia faida.

## KIFUNGU CHA II

**MADHUMUNI**

Yafuatayo ndiyo madhumuni ya **CHAKITA:**

Kuendeleza usomi wa lugha ya Kswahili kisayansi na kitaaluma katika vipengele vyake vyote.

Kushirikisha lugha, fasihi na isimu ya Kiswahili kama masomo ya kiakademia katika taasisi za elimu ya juu na nyingine zozote zitakazohitaji ushirikishi huo.

Kushirikisha lugha ya Kiswahili kama chomho cha maendeleo ya kitaifa; na uhifadhi, pamoja na uendelezaji wa utamaduni.

Kufundisha na kuiratibu lugha ya Kiswahili kama chombo cha ustawi na maendeleo endelevu pamoja na ustaarabu mwafaka katika jamii.

Kuwezesha ufanyikaji wa utafiti kuhusu maswala muhimu katika lugha, isimu na fasihi ya Kiswashili.

Kuwezesha ushirikiano wa kiakademia, huduma za ushauri na kushiriki katika shughuli za kijamii na kitamaduni ili kuongoza mijadala kuhusu hali halisi katika maswala ya lugha ya Kiswahili.

Kujenga uhusiano wa kuwili wa kusaidiana na kuchagizana baina ya elimu ya Kiswahili na shughuli nyingine za kijamii na kitamaduni pamoja na taaluma nyingine ili kuibua mfumo wa taaluma mbalimbali kuchangia maarifa.

## KIFUNGU CHA III

**Shughuli**

**CHAKITA** Kitafanya yafuatayo:

a. Toa nafasi ya mijadala kuhusu vipengele vyote vya usomaji na ufundishaji wa lugha ya Kiswahili katika hali zake zote nchini Kenya.
b. Jitahidi kuimarisha na kushirikisha utafiti wa kiisimu kuhusu lugha ya Kiswahili na kuchapisha na kusaidia katika uchapishaji wa tafiti kama hizo inapowezekana.
**c.** Chapisha jarida litakaloitwa **TAALUMA.**

**d.** Anzisha na dumisha mawasiliano na ushirikiano na makundi halali yaliyo na maslahi sawa au yanavofanana na ya **CHAKITA.**

**e.** Jihusisha na shughuli nyingine ambazo, kulingana na maoni ya Kamati Kuu ya **CHAKITA,** zinaendeleza madhumuni ya **CHAKITA.**

f. Andaa mikutano, makongamano na warsha pamoja na semina mara nyingi iwezekanavyo.

## KIFUNGU CHA IV

### Viwango vya Uanachama

Kutakuwa na viwango sita vya uanachama:

1. **Wanachama waanzilishi:**

   Idara zifuatazo za lugha katika vyuo vikuu nchini Kenya (zitakazoitwa idara anzilishi) zitajulikana kama wanachama waanzilishi wa **CHAKITA.**

   a. Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret.

   b. Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Nairobi.

   c. Lugha na Isimu, chuo kikuu cha Egerton, Njoro.

   d. Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Maseno, Maseno.

   e. Lugha na Fasihi, Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki, Baraton.

2. **Uanachama Jumuishi**

   Utatolewa kwa idara za vyuo vikuu na mashirika mengine mbali na zile za vyuo vianzilishi zitoapo maombi ambayo lazima yakubalike na wanachama wa **Chakita.** Maombi hayo yatahitaji kuungwa mkono na thuluthi mbili ya wingi wa kura

itakayopigwa na wanachama katika Mkutano Mkuu wa **CHAKITA** ama kwa kura kupitia posta.

**3. Uanachama Kamili**

Utatolewa kwa wanachama wote wa idara anzilishi pamoja na wanachama jumuishi.

**4. Uanachama wa Heshima**

Utatolewa na Kamati Kuu kwa watu binafsi ambao wametoa mchango wa kutajika katika uendelezaji wa madhumuni ya **CHAKITA.**

**5. Uanachama wa Kudumu/Maisha**

Utatolewa kwa uamuzi wa Kamati Kuu kwa watu binafsi wanaotoa michango mikubwa ya fedha na mali nyingine kwa **CHAKITA.**

**6. Uanachama Shiriki**

Utatolewa kwa watu binafsi na mashirika ambayo hayana uanachama katika hivyo viwango vingine.

## KIFUNGU CHA V

**Haki na Wajibu wa Wanachama**

**A. Wanachama Anzilishi**

1. Wanachama Anzilishi wana haki za uanachama katika kategoria hii.
2. Kila idara/chuo anzilishi kina haki ya kuwa na jina lake katika orodha ya wanachama anzilishi katika karatasi yenye anwani rasmi ya **CHAKITA.**
3. Kila idara anzilishi ina haki ya kupata nakala moja ya machapisho yote ya **CHAKITA** kwa bei sawa na ile va Wanachama Kamili.

4. Kila idara anzilishi ina haki ya kuteua mmoja wao kuwa mwakilishi katika Kamati Kuu ya **CHAKITA** kulingana na KIFUNGU CHA VII hapa chini.
5. Kila idara anzilishi ina haki ya kuchagua mmoja wao kufanya kazi katika Bodi ya uhariri ya chapisho la **Chakita** kulingana na KIFUNGU CHA XV D, hapa chini.
6. Kila idara anzilishi ina haki ya kumuondoa mwakilishi wake katika Kamati Kuu na Bodi ya Uhariri, muradi mwingine ameteuliwa, kulingana na KIFUNGU VII E.
7. Kila idara anzilishi ina wajibu wa kuipa Kamati Kuu ya **Chakita** orodha kamili ya wanachama wake na kuifahamisha panapotokea mabadiliko katika uanachama wake.
8. Kila idara anzilishi ina wajibu wa kugharimia usafiri na malazi ya mwakilishi wake aendapo kuhudhuria mikutano ya Kamati Kuu iwapo Kamati Kuu haina uwezo huo. Ipatapo fedha zozote kwa minajili hiyo, Kamati Kuu itazigawa sawa miongoni mwa idara zote.
9. Kila idara anzilishi ina wajibu wa jumla wa kushirikiana.

**B. Wanachama Jumuishi:**

Wana haki na wajibu sawa na wanachama anzilishi, isipokuwa, hawatakuwa na haki zilizoelezwa katika KIFUNGU V A, 1 hapo juu.

**C. Wanachama Kamili:**

1. Wanachama Kamili wana haki ya kuchangia katika jarida la **Chakita, TAALUMA** na kuelezwa kuhusu machapisho mengine ya **Chakita** na kuyanunua.
2. Wanachama Kamili wana haki ya kushiriki katika shughuli zote za **Chakita,** ikiwa ni pamoja na makongamano, warsha, semina, mikutano nk. kulingana na masharti yoyote yatakayotolewa na Kamati Kuu ama moja kati ya kamati zake.
3. Wanachana Kamili wanawajibika kulipa ada zao za uanachama katika robo ya kwanza ya kipindi cha mwaka wa fedha uanzao Januari Mosi hadi Disemba 31.
4. Wanachama kamili wana wajibu wa jumla wa kushirikiana kikamilifu katika shughuli za **Chakita** na kujitolea kwa malengo yake.

**D Wanachama wa Heshima:**

1. Wanachama wa Heshima watakuwa na haki zote walizonazo Wanachama kamili.

**E Uanachama wa Kudumu/Maisha:**

1. Wanachama wa Kudumu/Maisha vvana haki ya kupata nakala ya jarida la taaluma bila malipo kwa kipindi chote cha maisha yao mradi jarida bado linachapishwa.

**F. Wanachama Shiriki:**

1. Wanachama Shiriki wana haki ya kulipa ada ya jarida la **Chakita, Taaluma.** Kujulishwa kuhusu machapisho mengine ya **Chakita** na kuyanunua.
2. Wanachama Shiriki wana haki ya kushiriki katika shughuli zote za **Chakita,** ikiwa ni pamoja na makongamano, warsha, semin, mikutano nk. kulingana na masharti yoyote yatakayotolewa na Kamati Kuu ama moja kati ya kamati zake.
3. Wanachama Shiriki wanawajibika kulipa ada zao za uanachama katika robo ya kwanza ya kipindi cha mwaka wa fedha kama ilivyoonyeshwa katika KIFUNGU 5B, 3 hapo juu.
4. Wanachama Shiriki wana wajibu wa jumla wa kushirikiana kikamilifu katika shughuli za **Chakita** na kujitolea kwa malengo yake.

## KIFUNGU VI

### Viongozi

Kamati Kuu itajumuisha mwakilishi mmoja kutoka kwa kila idara anzilishi na mashirika yaliyojumuishwa. Wawakilishi hawa watateua Mwenyekiti na Katibu pamoja na Mweka Hazina miongoni mwao kulingana na mahitaji ya chama. Kando na Mwcnyekiti, kama ilivyoelezwa katika KIFUNGU VIII, A, W, kila mwanachama wa Kamati Kuu atakuwa na kura moja tu katika shughuli za **Chakita.**

## KI FUNGU VII

### Kamati Kuu

A. Chama cha **Chakita** kitatawaliwa na Kamati Kuu iliyo chombo chake cha kuunda na kutekeleza sera.

B. Kamati Kuu inajumuisha mwakilishi mmoja kutoka kwa idara anzilishi na jumuishi.

C. Mwenyekiti atakuwa kinara wa **Chakita** na Kamati Kuu yake.

D. Wanachama wa Kamati Kuu watachaguliwa kushikilia nyadhifa zao kwa kipindi cha miaka miwili. Watachaguliwa kwa wingi wa kura katika idara zao mbalimbali.

E. Viongozi wote katika Kamati Kuu watachaguliwa kwa wingi wa kura.

F. Kamati Kuu yaweza kuchagua kamati mbalimbali na kushirikisha wanachama wapya wasiozidi wanne, kwa minajili fulani kulingana na mahitaji ya chama. Wanachama wa kamati kama hizo pamoja na wanachama walioshirikishwa hawatakuwa na haki ya kupiga kura katika mikutano ya Kamati Kuu.

G. Wanachama wote wa Kamati Kuu watakuwa wanachama wa Kudumu/Maisha wa **Chakita.** Yeyote anayekoma kuwa mwanachama wa idara anzilishi na mashirika jumuishi anatoka kwa Kamati Kuu mara moja. Likitukia hilo, idara anzilishi au jumuishi husika itawajibika kuteua mwakilishi mwingine kabla ya siku tisini kupita. Aya hii inahusu pia uanachama kwa Kamati ya Uhariri.

H. Kamati Kuu itakutana wakati na mahali itakapoamua. Ni lazima ikutane angalau mara moja kwa mwaka.

I. Mradi wanachama wote wamepewa arifa ya mkutano kwa wakati unaofaa, kutahitajika wanachama watatu kuwa na akidi. Mmoja kati ya hao watatu lazima awe; Mwenyekiti, Katibu ama Mweka Hazina.

J.Kila wadhifa unapokuwa wazi utajazwa na Kamati Kuu haraka iwezekanavyo.

K. Kamati Kuu itaidhinisha usajili wa wanachama wapya. Wanachama wapya katika kundi la shirika jumuishi watahitaji kutimiza maelezo ya KIFUNGU VII, 7, E, hapo juu.

L. Kamati Kuu itakuwa na uwezo wa kubadilisha kiwango cha ada ya mwaka inayolipwa na wanachama wa **Chakita**.

## KIFUNGU VIII

### Majukumu ya Viongozi

**A. Mwenyekiti:**

1. Ataongoza mikutano yote ya Kamati Kuu na mikutano mingine yote ya **Chakita** atakayohudhuria. Wakati hayupo, mmoja wa wanachama wa Kamati Kuu aliyepo atachaguliwa kushikilia.
2. Atakuwa na kura ya pili pande mbili au zaidi zinazopingana zikilingana katika upigaji kura. Mwenyekiti asipokuwepo, anayeshikilia atakuwa na haki hiyo.

**B. Katibu:**

1. Atayashughulikia mawasiliano rasmi yote ya **Chakita**.
2. Atakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi yake mwenyewe anavyoona bora katika mambo ya dharura iwapo wanachama wengine wa Kamati Kuu hawawezi kupatikana

kwa urahisi. Hata hivyo, maamuzi kama hayo yatahitaji kuidhinishwa katika mkutano ufuatao wa Kamati Kuu.

**3.** Ataandaa na kusambaza kumbukumbu za mikutano yote ya Kamati Kuu na mikutano mingine ya **Chakita.**

**4.** Atakuwa na jukumu la kuhifadhi na kutunza rekodi, vifaa na mali yote ya **Chakita.**

**5.** Atapaswa kuwasiliana na wanachama wa Kamati Kuu kuhusu shughuli zote za **Chakita.**

**C. Mweka Hazina:**

1) Atapokea na kutumia fedha za **Chakita** kufuatana na maagizo ya Kamati. Aidha. atahitajika kutoa risiti kwa pesa zote anazozipokea na kuhifadhi hati za malipo za pesa anazozitumia.

**2)** Anawajibika kuhifadhi vizuri na kutoa kwa Kamati Kuu pamoja na wanachama wa **Chakita** akaunti zote za **Chakita.**

**D. Katibu/Mweka Hazina:**

1. Atatekeleza shughuli za uhusiano mwema kwa niaba ya **Chakita** kwa mashauriano na Mwenyekiti.
2. Atakwa na haki ya kutoa baadhi ya majukumu yake kwa kiongozi mwingine ama kwa Kamati Kuu ya **Chakita** kwa idhini ya Kamati Kuu ambayo itahitajika kuyataja bayana majukumu hayo.

## KIFUNGU IX

**Uteuzi**

Mbali na uteuzi wa kamati mbalimbali na wanachama jumuishi, kulingana na KIFUNGU 7, F, Kamati Kuu ina nguvu za kuteua mhariri, Katibu Mkuu na wadhamini kwa kipindi cha miaka miwili.

**A Mhariri**

1. Atashauriwa katika uandalizi wa sera za uhariri na mipango mingine ya jarida la TAALUMA
2. Ana jukumu la kutekeleza sera za chama kuhusiana na **TAALUMA** na machapisho mengine yote ya **Chakita.**
3. Hapaswi kuwa mwanachama wa Kamati Kuu.

**B Katibu Mkuu:**

1. Atakuwa na wajibu wa kutekeleza sera na mipango mbalimbali ya **Chakita** kwa uelekezi wa Kamati Kuu.
2. Atashauriwa katika maandalizi ya sera na mipango ambayo itakuwa sehemu ya majukumu yake.
3. Hatakuwa mwanachama wa Kamati Kuu.

## KIFUNGU X

**Mikutano Mikuu**

**Chakita** kitakuwa na aina mbili za mikutano mikuu: Mikutano Mikuu ya Kawaida na Mikutano Mikuu Maalum.

**A. Mikutano Mikuu ya Kawaida:**

1. Utaandaliwa mara moja kila baada ya miaka miwili.
2. Utahitaji arifa kwa maandishi itakayoambatana na maelezo ya matumizi ya pesa za chama kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita pamoja na ajenda ya mkutano ujao. Arifa hiyo itahitaji kutolewa kwa wanachama wote mwezi mmoja kabla ya tarehe ya mkutano na inapowezekana kutolewe taarifa katika magazeti angalau siku ishirini na moja kabla ya tarehe ya mkutano.
3. Uwe na ajenda ambayo itahusisha yafuatayo:

a. Ushahidi kuwa kumbukumbu za mkutano uliopita zimethibitishwa.
b. Ripoti zilizotolewa na Mwenyekiti, Katibu/Mweka Hazina na Mhariri.

c. Hali ya vitabu vya pesa za **Chakita** pamoja na ripoti ya mkaguzi wa mahesabu.

d. Uteuzi wa mkaguzi wa mahesabu wa miaka miwili inayofuata.

e. Mambo mengine yatakayoamuliwa na Kamati Kuu pamoja na ambayo mwanachama ama wanachama watakuwa wametoa kwa maandishi kwa Katibu angalau wiki tatu kabla ya tarehe ya mkutano.

f. Maswala mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti.

g. Kusimikwa kwa Kamati Kuu mpya.

## B. Mikutano Mikuu Maalum:

1. Utaitishwa kwa sababu yoyote maalum kwa kura ya sehemu nne ya tano ya wanakamati kuu.
2. Utahitaji arifa kutolcwa kwa wanachama wote angalau wiki nne kabla ya tarehe ya mkutano na inapowezekana kuwe na tangazo katika magazeti angalau wiki mbili kabla ya tarehe ya mkutano huo.
3. Utaitishwa haraka iwezekanavyo mara Kamati Kuu ipatapo ombi kwa maandishi kutoka kwa wanachama kamili wasiopungua thelathini ama kutoka kwa angalau idara anzilishi ama jumuishi mbili.

**KIFUNGU XII**

## Mdhamini

Shamba, majengo, mali nyingine isiyoweza kuhamishwa hamishwa, vitega uchumi na amana zote za **Chakita** zitawekwa kwa jina la mdhamini ama wadhamini watakaoteuliwa na Kamati Kuu kulingana na KIFUNGU 10,B,C,D,F,HG,H,I hapo juu.

**KIFUNGU XIII**

## Mkaguzi wa Hesabu

### A. Mkaguzi wa Hesabu:

1. Atateuliwa kutoka nje ya uanachama wa **Chakita** kwa kipindi cha miaka miwili katika kila Mkutano Mkuu wa Kawaida.

2. Atakuwa na haki ya kukagua akaunti, rekodi na stakabadhi zote za **Chakita** wakati wowote.
3. Atakuwa na haki ya kuomba maelezo kamili ya vitabu vya hesabu vya **Chakita** kutoka kwa Katibu ama Mweka Hazina kila mwaka. Hili litafanyika wakati wowote mradi si chini ya wiki sita wala zaidi ya miezi mitatu kabla ya kila Mkutano Mkuu wa Kawaida.
4. Akishapata vitabu hivyo na kuvikagua atapaswa kueleza kama viko katika hali nzuri kulingana na sheria ama atoe ripoti kwa Mwenyekiti na Wanachama wa **Chakita** ni vipi visivyo katika hali inayokubalika.

B. Nakala ya ripoti ya Mkaguzi wa Hesabu kuhusiana na akaunti za chama pamoja na maelezo kuhusu akaunti hizo itatolewa kwa wanachama wote wakati wa kutoa arifa ya kuitisha Mkutano Mkuu wa Kawaida. Mkaguzi wa Hesabu atalipwa kiwango cha tuzo kwa kazi yake kitakachoamuliwa na Mkutano Mkuu wa Kawaida uliomteua.

**KIFUNGU XIV**

## Hazina

A. Matumizi ya hazina ya **Chakita** yataongozwa na Kamati Kuu kwa wingi wa kura kwa madhumuni yafuatayo:

1. Gharama za ukatibu;
2. Gharama za uhariri na uchapishaji;
3. Makongamano;
4. Usafiri muhimu;
5. Gharama nyingine muhimu.

B. Pesa zote zitapokelewa na Katibu ama Mweka Hazina kwa niaba ya **Chakita** na kutunzwa naye kwa jina la **Chakita** katika akaunti zilizoidhinishwa na Kamati Kuu itakayoamua namna akaunti hiyo itakavyoendeshwa.

C. Kamati Kuu itaweka kiwango cha pesa ambacho hakiwezi kuzidishwa katika malipo yanayofanywa kwa niaba ya chama bila idhini ya Mwenyekiti.

D. Hundi zote zitakazoandikwa kwa niaba ya **Chakita** zitawekwa sahihi na Mwenyekiti, Katibu, na Mweka Hazina ama mwanakamati mwingine aliyeamuliwa na Kamati Kuu.

E. Kamati Kuu itaamua kiwango fulani cha pesa taslimu ambacho chaweza kuwa kwa hifadhi ya Katibu na /au Mweka Hazina. ama mtu mwingine aliyeamuliwa na Kamati Kuu mradi matumizi ya pesa hiyo yaweze kutolewa maelezo mema wakati wote.

F. Kamati Kuu itakuwa na nguvu za kumsimamisha kwa muda mwanachama yeyote anayeonekana kuwa hatumii vizuri pesa au mali ya **Chakita**. Idara anzilishi husika itafahamishwa kuhusu hatua hiyo ya kusimamishwa ili itoe ushauri kuhusu hatua nyingine ya kuchukuliwa.

**KIFUNGU XV**

## Jarida na machapisho mengine ya Chakita

A. Sera zote kuhusiana na jarida na machapisho mengine zitaamuliwa na Kamati Kuu na taarifa ya makubaliano kati ya **Chakita** na mchapishaji. Makubaliano hayo yaweza kujadiliwa upya bila uhitaji wa kubadilisha katiba hii.

B. Akaunti itafunguliwa kwa jina la jarida, **TAALUMA**, la **Chakita** na kuendeshwa na makubaliano ya **Chakita** na Mchapishaji.

**C.** Mhariri atakuwa na jukumu la kuamua makala zitakazochapishwa kulingana na sera za **Chakita.**

D. Mhariri anaweza kusaidiwa na mhariri msaidizi atakayemchagua na mhariri mshiriki kuchaguliwa na kila moja kati ya idara anzilishi na jumuishi kwa kipindi cha miaka miwili. Uchaguzi huu waweza kubatilishwa kulingana na KIFUNGU V, A (6).

**E.** Kutakuwa na bodi ya uhariri kumshauri na kumsaidia Mhariri kuhusu maswala ya jarida na machapisho mengine ya **Chakita.**

F. Bodi ya Wahariri itajumuisha wafuatao:

1. Mhariri, atakayekuwa Mwenyekiti wa Bodi.
2. Mhariri Msaidizi iwapo atateuliwa.

3. Wahariri Washiriki watano.
4. Mwenyekiti wa **Chakita** au mwakilishi wake atakayeteuliwa kutoka kwa wanakamati ama Wahariri Washiriki.
5. Wanachama wengine wa **Chakita** wasiozidi watano wawezao kushirikishwa katika Bodi ya Uhariri. Hawa hawatakuwa na nguvu za kupiga kura na watashikilia wadhifa huo kwa kipindi kitakachoamuliwa na Bodi lakini kisichozidi kile cha Mhariri.

**KIFUNGU XVI**

## Makao na Mali

A. Makao ya **Chakita** yatakuwa jijini Nairobi, Kenya.
B. Mali ya **Chakita** itatokana na ada ya usajili na ruzuku, mirabaha na misaada iliyokubaliwa na Kamati Kuu kwa matumizi yanayokubaliana na malengo ya **Chakita**.

## KIFUNGU XVII

## Ada za Uanachama

A. Kamali Kuu itatoa maamuzi kuhusu ada ya mwaka kwa aina mbalimbali za uanachama.
B. Ada ya uanachama sharti ilipwe katika robo ya kwanza ya mwaka la sivyo uanachama utasimamishwa.

## KIFUNGU XVIII

## Kuvunjika kwa Chama

A. **Chakita** chaweza kuvunjwa kwa uamuzi wa kura itakayoungwa mkono na thuluthi mbili za wanachama katika Mkutano Mkuu.Wanachama wasioweza kuhudhuria mkutano huo waweza kupiga kura kwa njia ya posta.
B. Iwapo **Chakita** kimevunjwa, mali ya **TAALUMA** itakayosalia baada ya kulipa madeni ya chama itatumika kulingana na maamuzi ya Kamati Kuu.

## KIFUNGU XIX

## Marekebisho ya Katiba

A. Marekebisho ya katiba ya **Chakita** yataamuliwa na thuluthi mbili za wanachama wanaopiga kura.

B. Wanachama watajulishwa kuhusu mapendekezo hayo ya marekebisho angalau mwezi mmoja kabla ya mkutano utakaoyajadili.

C. Wanachama ambao hawataweza kuhudhuria mkutano huo wanaweza kupiga kura kwa njia ya posta.

D. Mambo yote ambayo hayajaelezwa wazi wazi katika katiba hii yataamuliwa na Kamati Kuu. Uamuzi huo ni sharti uripotiwe kwa Mkutano Mkuu ufuatao ili kuratibishwa.

## KIFUNGU XX

## Ukaguzi wa Vitabu na Orodha ya Wanachama

Mwanachama yeyote wa **Chakita** ataruhusiwa kukagua orodha ya wanachama, akaunti na stakabadhi nyingine zote za chama katika makao ya chama, mradi ombi la kufanya hivyo kwa maandishi limepokelewa na Katibu au Mweka Hazina siku saba kabla ya siku iliyopendekezwa kwa shughuli hiyo.